MKATABA WA KUPANGISHA
GEREJI

Baina ya

NAS HAULIERS LIMITED

Na

AHMED NAS LTD

IMETAYARISHWA NA:-

MUSTAFA ADVOCATES
P.O. Box 5412
TANGA.

MKATABA WA KUPANGISHA GEREJI

Mkataba wa kupangisha Garage iliyopo Kiwanja 454 & 456 Kange Industrial - jiji la Tanga, umefanyika leo tarehe 01 mwezi wa 01, 2022 kati ya **NAS HAULIERS LIMITED** wa S.L.P, Tanga ambaye katika Mkataba huu atafahamika kama "Mwenye Gereji" na **AHMED NAS LTD** wa S.L.P 1087, Tanga ambaye katika mkataba huu atafahamika kama "Mpangaji" kwa masharti yafuatayo:-

1. Kwamba mkataba ni wa miaka mitano (5) na utaanza tarehe 01 mwezi wa 01, 2022 hadi tarehe 31 mwezi wa 12, 2027.

2. Kwamba kodi kwa mwezi ni **Tshs. 1,000,000/=** na Mpangaji atakuwa akimlipa mwenye Gereji kila baada ya mwaka mmoja ataoa kiasi cha Tshs **12,000,000/=.**

3. Kwamba Mpangaji amekabidhiwa Gereji hiyo na ataitumia kwa biashara ya kutengeneza magari.

4. Kwamba Mpangaji atatunza Gereji hiyo na sehemu zote zinazohusika na mkataba huu bila kusababisha uharibifu wowote.

5. Kwamba Mpangaji haruhusiwi kumpangisha mtu mwingine yeyote ndani ya Gereji hiyo, na endapo atafanya hivyo, atakuwa amevunja mkataba huu na Mwenye Gereji atakuwa huru kuchukua Gereji yake.

6. Kwamba bili za umeme na bili za maji zitakuwa zikilipwa na Mpangaji. Kodi ya kiwanja na *propertytax* italipwa na Mwenye Gereji.

7. Kwamba Mwenye Gereji anaweza kwa majadiliano kupandisha kodi ya mwezi kabla ya mkataba kumalizika.

8. Kwamba mwisho wa Mkataba huu Mpangaji na Mwenye Gereji wanaweza kuingia kuingia katika mkataba mwingine kwa maelewano yao tena.

9. Kwamba endapo Mpangaji atapenda kuhama au Mwenye Gereji hatapenda kuendelea na Mkataba, basi kila mmoja wao itampasa kutoa notisi ya miezi mitatu kabla ya tarehe iliyokusudiwa.

KAMA ishara ya hiari zao wahusika wanatia saini zao hapa chini kama ifuatavyo:-

NAS HAULIERS LIMITED (Mwenye Gereji)

Jina la Mkurugenzi: ALLI HEMED ABDALLAH

Saini.....Tarehe: 01/01/2022

Muhuri

NASHAULIERSLTD
P.O.Box 5622
DAR-ES-SALAAM

.....

AHMED NAS LTD (Mpangaji)

Jina la Mkurugenzi: AHMED HEMED ABDALLAH

Saini.....Tarehe: 01/01/2022

Muhuri

AHMED NAS LTD
P.O. Box 4261
DAR ES SALAAM

.....

IMETOLEWA NA KUTIWA SAINI MBELE YA:
MUSTAFA ADVOCATES
P.O. Box 5412
Tanga

Saini.....

Cheo: WAKILI

Tarehe: 01/01/2022

MUSTAFA RAJABU MLAWA
ADVOCATE
P.O Box 5412
TANGA
NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS